



COVID -19 MUONGOZO WA UTUMAJI TAARIFA NA UTANGAZAJI TOKEA NYUMBANI

YALIYOMO

1. UTANGULIZI	4
JINSI YA KUTUMIA MUONGOZO HUU	5
MALENGO YA MUONGOZO HUU	5
TAFSIRI	5
KUTOA TAARIFA ZA COVID-19 KWA UWAJIBIKAJI	8
2. MATAYARISHO YA MSINGI - KUTAYARISHA KIPINDI CHAKO CHA REDIO	9
Ugawaji majukumu na wajibu katika kikundi/timu	9
Kikao cha kutayarisha kipindi tokea nyumbani	11
Kupata wageni wa kipindi unapotoa taarifa tokea nyumbani	12
	13
3. KUTOA TAARIFA TOKEA NYUMBANI	
TAFSIRI	13
Kujifunza kutumia simu ya mkononi kama zana ya kutoa taarifa	13
Kujirekodi	14
Kurekodi mahojiano na mtu asiye chumbani nawe	
Uzoefu bora wa matumizi ya WhatsApp	15
Kanuni za kurekodi mahojiano kupitia ujumbe wa sauti	16
Miongozo na mazingira ya kurekodi	17
Kuandika orodha ya kilichorekodiwa	18
MIUNDO YA VIPINDI VYA REDIO	18
Mahojiano	18
Sauti ya Umma	20
Wasifu wa Sauti	20
Maoni ya Sauti	21
Taarifa kutoka enelo la tukio	22

Muongozo huu umetengenezwa na Children's Radio Foundation kwa kushirikiana na UNICEF ya Afrika ya Kusini (UNICEF South Africa)

Kumbukumbu za sauti	23
Je, Wajua	24
Kufungua na kufunga miundo ya redio	25
Kushirikisha wasikilizaji kupitia mitandao ya kijamii	25
Jaribio	26
Kujibu maswali ya wasikilizaji	26
Kutafuta mada mahususi kutoka kwenye mitandao ya kijamii	28
4. BAADA YA MATAYARISHO YA KIPINDI NA UTANGAZAJI TOKEA NYUMBANI	29
Viungo vya Kipindi Cha Redio na Kuhifadhi	31
Viungo vya Kipindi cha Redio	
Kuhifadhi kwenye SoundCloud	32
5. SHUKRANI	33
6. RASILIMALI	

Muongozo huu umetengenezwa na Children's Radio Foundation kwa kushirikiana na UNICEF ya Afrika ya Kusini (UNICEF South Africa)

1. UTANGULIZI

JINSI YA KUTUMIA MUONGOZO HUU

Kama unavyoweza kuona, 2020 inageuka kuwa mwaka wa kushangaza zaidi kwa ulimwengu kwa sababu kila bara, nchi, jamii, kaya na mtu anajaribu kuelewa hali halisi ambayo janga la COVID-19 limesababisha.

Katika nchi nyingi, hatua muhimu kama vile za kudumisha umbali wa kijamii na kusimamisha shughuli ili kukomesha kuenea kwa maambukizi zimetokelezwa ili kuhakikisha usalama wako. Ingawa vizuizi hivi vinaweza kuwa havikuwekwa katika kila eneo nchini mwako, kesi zilizobainiwa za maambukizo ya COVID-19 zimetambuliwa kila mahali.

Huu ni wakati muhimu na ulimwengu unahitaji hadithi/simulizi na tafakari za vijana zijumuishwe kwenye ajenda yake. Maamuzi, mikakati, na mipango ambayo inatengenezwa sasa itaunda hatima yako na kwa hivyo sauti yako ni muhimu kwa wakati huu.

Sio muhimu tu kukuza sauti ya jamii, lakini pia kama wanahabari vijana, ni jukumu lenu kuhakikisha kuwa taarifa sahihi zinafikia jamii yako. Muongozo huu umeundwa kukusaidia kufanikisha hilo kwa usalama.

Muongozo huu una alama za ishara chache ambazo zitaonekana kote. Zinamaanisha:



KIDOKEZO: Ushauri mdogo



KWA MFANO: Dhana inayoelezea jambo fulani



REJEA: Rudi nyuma na uangalie sehemu iliotangulia

MALENGO YA MUONGOZO HUU

Childrens Radio Foundation (CRF) hivi sasa hufundisha wanahabari vijana katika vituo 68 vya redio katika nchi sita za Afrika (Jamhuri ya Kidemokrasia ya Kongo, Liberia, Ivory Coast , Afrika Kusini, Tanzania, na Zambia) kutoa vipindi vya redio kila wiki na shughuli za kijamii kila mwezi.

Unafanyia kazi mada kama vile mabadiliko ya tabia nchi, afya ya kijinsia na uzazi, elimu, uhamiaji, vurugu na usalama wa jamii, na mengine. Unachukua wasikilizaji wa kipindi cha redio na washiriki wa shughuli za kijamii kwenye safari muhimu ya kuelewa changamoto mbali mbali zinazoikabili jamii yako. Kwa kweli tunajivunia alama ambayo umeiweka kupitia mazungumzo haya, na tusingetaka hiyo isimame sasa.

Kuripoti kuhusu mada yoyote huhitaji utunzaji na uwajibikaji, kutoa taarifa kuhusu COVID-19 inahitaji hili zaidi.

Muongozo huu una malengo matatu makuu:

1. kuzingatia COVID-19 na kuipa kipaumbele katika ajenda yako
2. kukujulisha kuhusu kuripoti na kutangaza vipindi tokea nyumbani na jinsi inavyofanywa
3. kukupa uwezo wa kupata vijana wengine na watu wazima katika jamii yako ambao wanataka kutoa hadithi/ simulizi zao za COVID-19

TAFSIRI

Kuripoti kwa uwajibikaji kuhusu COVID-19 inabidi uelewe maneno kadhaa muhimu yanayotumiwa sana. Hapa chini kuna orodha na ufafanuzi unaohitaji kujielimisha mwenyewe wakati unatuma taarifa za COVID-19.

- **Virusi vya Corona, yaani Coronaviruses (CoV)** ni familia kubwa ya virusi ambavyo husababisha magonjwa kwa wanyama na binadamu. Magonjwa haya huanza kama homa ya kawaida na kuwa ugonjwa mkali wa mfumo wa upumuaji kama vile 'Middle East Respiratory Syndrome' au (MERS-CoV) na 'Severe Acute Respiratory Syndrome' au (SARS-CoV) ([National Institute of Allergy and Infectious Diseases](#)).
- **Virusi vipya vya korona** (novel Coronavirus, yaani nCoV) ni aina mpya

ambayo haijatambuliwa awali katika binadamu ([Shirika la Afya Duniani](#)).


- **COVID-19** ni ugonjwa wa kuambukiza unaosababishwa na virusi vya corona vilivyogunduliwa hivi karibuni tu. Virusi hivi vipya na ugonjwa huu haukujulikana kabla ya mlipuko wa ugonjwa ulioanza Wuhan, China, mnamo Desemba 2019 ([Shirika la Afya Duniani](#)).
- **Mlipuko wa ugonjwa** ni kupanda ghafla kwa idadi ya matukio ya ugonjwa fulani. Mlipuko wa ugonjwa unaweza kutokea katika jamii au eneo la kijiografia, au unaweza kuathiri nchi kadhaa. Unaweza kudumu kwa siku chache au wiki, au hata kwa miaka kadhaa. Mlipuko kadhaa inatarajiwa kila mwaka, kama vile homa ya kawaida ([APIC.org](#)).

- **Janga** (epidemic) hutokea wakati ugonjwa wa kuambukiza huenea kwa kasi kwa watu wengi. Mnamo 2003, ugonjwa hatari wa kupumua wa 'SARS' uliua watu karibu 800 ulimwenguni kote (APIC.org).
- **Janga kuu** (pandemic) ni mlipuko wa kimataifa wa ugonjwa fulani. Inatofautiana na mlipuko au janga (epidemic) kwa sababu:
 - huathiri eneo kubwa la kijiografia, mara nyingi ulimwenguni kote;
 - huambukiza idadi kubwa ya watu kuliko janga la ndani ya nchi;
 - mara nyingi husababishwa na virusi vipya au aina ya virusi ambavyo haivijazunguka kwa watu kwa muda mrefu, binadamu kawaida huwa hawana kinga yoyote, au ya kutosha, dhidi yake; Virusi huenea haraka kutoka kwa mtu moja hadi mwingine ulimwenguni;
 - husababisha idadi kubwa ya vifo kuliko magonjwa ya janga (epidemics); na
 - mara nyingi husababisha usumbufu wa kijamii, upotezaji wa kiuchumi, na ugumu kwa ujumla. (APIC.org).
- Watu huwekwa katika **hali ya kutokaribiana** (karantini) wakati bado hawajakuwa wagonjwa, lakini wanaweza kuwa wamepata tishio la kufikiwa na mambukizi ya ugonjwa fulani, kama vile COVID-19. Hii inaweza kusaidia kukomesha kuenea kwa ugonjwa huo. Watu hupunguza mawasiliano na wengine ili kuruhusu kipindi wameanza kupata COVID-19 (wakati unaoanza kupata maambukizi hadi kuonekana kwa dalili) ambayo ni kati ya siku 2 hadi 14. Ikiwa mtu ana dalili wakati huu, atahitaji kupimwa. ([Vituo vya Kudhibiti na Kuzuia Magonjwa, Taasisi ya Kitaifa ya Magonjwa Yanayoweza Kuambukizwa](#)).
- **Kujitenga karantini** (self-quarantine) ni hatua nyingine ya kinga kwa watu ambao wamekuwa kwenye hatari kubwa ya COVID-19 kama vile wale walio nchi za Uhispania, USA au Italia au wamewasiliana na mtu yeyote ambaye amesafiri kwenda nchi hizi. Kukaa nyumbani, badala ya kwenda shuleni au kazini na kuondoka tu wakati inapohitajika kabisa, kwa mfano, kununua chakula. Orodha ya nchi zilizo katika hatari kubwa hubadilika kila siku, na unaweza kutazama orodha hio kwenye ukurasa wa Shirika la Afya Duniani. Vituo vya Udhhibiti na Magonjwa, Shirika la Afya Duniani: ([Vituo vya Udhhibiti wa Magonjwa \(CDC\) na Uzuiaji, Shirika la Afya Duniani \(WHO\)](#)).
- **Kutengwa** (isolation) hufanyika wakati mtu ameambukizwa ugonjwa wa kuambukiza, na kutengwa mbali na watu wengine walio na afya nzuri. Hii pia husaidia kukomesha kuenea kwa ugonjwa huo ([Vituo vya Udhhibiti wa Magonjwa, CDC](#)).
- **Kujifungia** (self-isolation) ni sawa na kujitenga (self-quarantine). Mtu huingia katika hali ya kujifungia mwenyewe wakati anaonyesha dalili kama mafua, na anaweza kudhibitisha kuwa amewasiliana na mtu aliyeambukizwa COVID-19. Wakati huu, ni lazima watu wapunguze mawasiliano na wengine na wawasiliane na mtaalamu wa matibabu ([Shirika la Afya Duniani , Idara ya Afya na Vituo vya Afrika Kusini vya Udhhibiti wa Magonjwa na Kuzuia](#)).
- **Umbali wa kijamii** (social distancing) ni pamoja na kutokwenda katika sehemu zilizojaa watu, na ambapo mawasiliano ya karibu na wengine yanaweza kutokea, kama vile vituo vya ununuzi, sinema, uwanja wa michezo na mikusanyiko yeyote ya watu. Dumisha umbali wa mita 2 kutoka kwa wengine inapowezekana. Hatua za 'umbali wa jamii' (social distancing) mara nyingi zinamaanisha kuachishwa kwa mikusanyiko mikubwa (kama mikutano, madarasa, na hafla za michezo), kuzuia usafirishaji wa wingi na kusafiri, na kufanya kazi kutoka nyumbani. Hii

hufanywa ili kupunguza kasi ya ugonjwa wa kuambukiza kama COVID-19 unavyoenea na pia kupunguza nafasi za kuwasiliana na mtu aliye na maambukizi **(Vituo vya Kudhibiti na Kuzuia Magonjwa)**.

- **“Kuupunguza mzunguko”**(flattening the curve) ni wazo kwamba hatua za kinga, kama kutengwa na umbali wa kijamii, zinaweza kusaidia kuchelewesha kuzuka kwa idadi ya kesi na kupatia hospitali wakati wa kutosha wa

kujiandaa ili kusimamia wagonjwa wanaoingia. Mzunguko wa juu unamaanisha kuna visa vingi vinatokea kwa wakati mmoja, wakati mzunguko uliolala (wa rangi ya bluu) unamaanisha kuwa visa/matukio ya ugonjwa huja kwa wakati tofauti tofauti (sio kwa mara moja). Ni tofauti kati ya hali ya mtu kuwa amelazwa hospitalini au kulazimika kutibiwa kwenye hema la kambi ya muda.



Chanzo: CDC, Drew Harris, Shukrani: Connie Hanzhang Jin/NPR

- **Kizuizi cha kutoka nje (lockdown)** ni itifaki ya dharura ambayo inazuia watu kuondoka katika eneo fulani. Kuzuia kuenea kamili kunamaanisha kuwa ni lazima ukae mahali ulipo na usitoke au kuingia kwenye jengo (au eneo lililotajwa) isipokuwa kwa kusudi muhimu tu. Hali hii kawaida inaruhusu watu kupata vifaa muhimu kutoka kwa maduka ya vyakula, ya dawa na benki, ili watu waweze kukidhi mahitaji yao ya msingi. Shughuli zote zisizo muhimu hubaki zimefungwa kwa kipindi chote cha kuzuia kuenea (economictimes.com).
- **Ukosefu wa kinga mwilini** (immunocompromised) inamaanisha watu walio na mfumo dhaifu wa kinga, na ambao hawana uwezo wa kupambana na mashambulizi kutoka kwa bakteria au virusi. Magonjwa kama

saratani, ugonjwa wa kisukari, VVU na TB, na aina ya matibabu ambayo watu hupata kutokana na hali hizi, yanaweza kuathiri mfumo wa kinga. Mimba pia inaweza kuweka wanawake katika hali ya hatari. Watoa huduma za afya wanachukua hatua zaidi kuwalinda wagonjwa wao wote kutoka COVID-19, haswa wale ambao wanaweza kuwa hawana kinga nzuri (health.usnews.com).

- **Vifaa vya kujikinga binafsi (Personal Protective Equipment, 'PPE')** humaanisha vitu au vifaa vilivyoundwa kuvaliwa na mtu binafsi kwa usalama dhidi ya hatari ya afya. PPE iliyopendekezwa kuvaliwa wakati huu wa milipuko wa COVID-19 ni barokoa (maski), glavu, miwani na gauni. Kuna uhaba wa PPE kwa wafanyakazi wa afya kote ulimwenguni na wanazihitaji

sana, kwa hivyo hakikisha kutumia vifaa hivi wakati tu vinapohitajika (**Vituo vya Kudhibiti na Kuzuia Magonjwa**).

- **'Nomophobia'** ni hali wa wasiwasi inayotokana na kukosa simu ya mkononi (yaani 'no-mobile-phone-phobia'). Ni kuwa na adha kwa simu yako ya mkononi au hofu ya kutokuwa na simu

yako ya mkononi. Wakati huu wa janga la COVID-19, kumbuka usizidishe matumizi ya simu yako ya mkononi kwani hii inaweza kuathiri afya yako ya akili. Jipe shughuli zingine kama vile kusoma, kupika au kutengeneza sanaa (**Sciencedirect.com**).



REJEA SEHEMU YA 6. RASILIMALI kwa vyanzo muhimu na vya kuaminika

KUTOA TAARIFA ZA COVID-19 KWA UWAJIBIKAJI

COVID-19 inatoa tishio kubwa kwa afya yetu na ni mada ambayo inahitaji kuzingatiwa sana. Kama mwanahabari mtoto/kijana, ni uangalie taarifa zako kwa makini kabla ya kuzitangaza ili uwapashe wasikilizaji wako habari sahihi na zenye umuhimu.

Hii ni mada hatari kuripoti kwa suala la afya yako. Usijaribu kufanya mahojiano ya uso kwa uso na mtu yeyote. Watu wanaweza kuwa wameambukizwa virusi bila kuonyesha dalili zozote.

- Ukweli dhidi ya hofu! Kumbuka, eneza ukweli badala ya hofu! Milipuko na magonjwa ni jambo la kutisha, lakini sisi tuna jukumu la kuwapa wasikilizaji wetu habari zilizo sahihi zaidi, na kwa kutumia mbinu ambazo haziwatishi na kusababisha hofu. Kwa mfano, ikiwa unataka kutaja idadi ya vifo ambavyo vimetokea ulimwenguni kutokana na mlipuko wa ugonjwa wa Korona (COVID-19), pia taja idadi ya watu wale waliopona. Hii itasaidia watu kuweka muktadha wa habari na haitawatisha. Pia, jaribu kila wakati kutoa maelezo ya

jinsi ambavyo watu wanaweza kujizuia ili wasipate maambukizi.

- Kuwa mwangalifu kuhusu jinsi unavyoongea kuhusu Korona (COVID-19) hewani. Usimcheke mtu anaposhiriki hadithi yake binafsi nawe. Hii inaweza kuchangia kuleta unyanyapaa na kusababisha watu wengine kwenye jamii yako kuupuuza ugonjwa au hata, wasifuate miongozo ya kujizuia.
- Kumbuka kuuliza watu waliodhibitishwa kuwa wagonjwa ikiwa wangependa kutumia jina halisi, au kama wangependa jina la siri, ili kuwahakikishia usiri.
- Kumbuka 'kuongeza chumvi kwenye taarifa' haikubaliki kamwe katika kutoa taarifa kuhusu mlipuko wa magonjwa. Tumia habari zilizo rasmi na ujaribu kurahisisha maelezo kwa wasikilizaji wako kadri uwezavyo.

2. MAANDALIZI YA MSINGI - KUTAYARISHA KIPINDI CHAKO

UGAWAJI MAJUKUMU NA WAJIBU KWA WANAKIKUNDI

Kutoa taarifa na utangazaji tokea nyumbani bado unahitaji jukumu sawa na kule kuripoti kwa uso kwa uso. Tofauti pekee iliopo ni kwamba majukumu mengine yatahitaji kuunganishwa au yataingiliana kwa sababu ya vizuizi vya kuingiliana uso kwa uso.

Chini ni muhtasari wa majukumu na kazi zinazohitajika ili kutoa taarifa na kutangaza kutokea nyumbani .

Mwanahabari/mhandisi wa sauti/

mtangazaji: Unapotengwa na washiriki wengine wa kikundi chako, kila mmoja atalazimika kujifunza kutekeleza majukumu yote tofauti peke yake ambayo kwa kawaida yangefanywa na watu tofauti. Utawajibika kuandaa, kupanga, na kurekodi miundo yote ya kipindi cha redio, kama vile mahojiano na sauti za umma. Pia utaonyesha wageni jinsi ya kuunda na kuwasilisha miundo yao ya redio kama maoni ya sauti, kumbukumbu za sauti (audio diary), na wasifu wa sauti. Kwa sababu wanahabari watafanya kazi moja kwa moja na sauti zilizorekodiwa na wageni wao wa kipindi, ni jukumu lao kuhakikisha ubora unaofaa wa sauti ya redio, kuweka kumbukumbu (logging) na kuhifadhi yote, na siku ya uwasilishaji, kumfikishia mwezeshaji kifurushi cha sauti kilichorekodiwa tayari . Kifurushi hiki kitatumika kutayarisha maandalizi ya kipindi cha mwisho cha radio cha dakika 30 hadi saa 1.

Jukumu la mwandishi/ mhandisi wa sauti ni:

- Kutafuta wageni na wachangiaji wa kipindi cha redio
- Kuandika scripti na rekodi vipindi:
 - [Maandishi ya kufungua na kufunga kipindi na kila kipengele \(miundo yote\)](#)

- Kukusanya taarifa za sehemu ya “je, wajua’ kwa ajili ya kipengele cha jaribio
- Kuandaa maswali ya mahojiano
- Kuandaa swali la kukusanya sauti za umma (vox pops)
- Kuwapa wageni maelezo kuhusu jinsi ya kutengeneza miundo ya redio inayohitajika na kuhakikisha kwamba miundo wanayotuma imefikia viwango vya ubora vya redio vinavyokubalika.

Mtayarishaji: Mtayarishaji hushirikisha na kusaidia wanahabari wengine wote kwenye kikundi kuhakikisha kwamba kila mtu anafanya kile anachokusudiwa kufanya ili kipindi kiwe tayari. Jukumu la mtayarishaji ni:

- Kuhakikisha kuwa ratiba ya wiki inazingatiwa na kuwasiliana na mwezeshaji ikiwa kuna ucheleweshaji wowote
- Kutengeneza ratiba ya mtiririko wa kipindi (show-clock)
- Kutengeneza ratiba ya mikutano ya kupanga utengenezaji wa kipindi na kikundi
- Kujaza fomu ya tathmini ya kipindi kila wiki baada kipindi cha redio na ushiriki wa mitandao ya kijamii
- Kuangalia kama kipindi kimehifadhiwa katika mtandao wa SoundCloud
- Kusimamia kikundi cha WhatsApp kilichoundwa kwa kila kipindi na kuwaarifu washirika kuhusu madhumuni ya kikundi hicho

Mtafiti: Baada ya mada, mada mahususi na vyanzo vya habari vimeamuliwa na kikundi, watafiti wanawajibika kutafuta taarifa zinazofaa ili kusaidia mwandishi/mhandisi wa sauti kuandika scripti yao, na kusaidia kuwafahamisha kuhusu machapisho kutoka kwenye mwandalizi wa mitandao ya kijamii.

Jukumu la mtafiti ni:

- Kusaidia mwandishi/mhandisi wa sauti kuandika scripti ya kipindi
- Kusaidia mwandishi/mhandisi wa sauti kutafuta simulizi au habari na wageni

Mtangazaji wa mitandao ya kijamii

(social media presenter): Mtangazaji wa mitandao ya kijamii anawajibika kushirikisha wasikilizaji kutumia mitandao ya kijamii. Kwa sababu kipindi chako kitakuwa kimerekodiwa tayari, wasikilizaji hawataweza kukupa maoni yao “moja kwa moja” kipindi kinaporushwa hewani. Kwa hivyo, maingiliano yote ya wasikilizaji yatafanyika kwenye mitandao ya kijamii inayofaa kama ile wasikilizaji wako wanapenda kutumia.

Jukumu la mtangazaji wa mitandao ya kijamii ni:

- Kushughulikia maandalizi ya moja kwa moja kwenye Facebook au Instagram ambapo mtashirikiana na wasikilizaji
- Kukusanya majibu ya jaribio na kutangaza mshindi wa juma hilo



Wasimamizi wa WhatsApp (WhatsApp

Admin): Rejea ukurasa wa “Ushiriki wa Wasikilizaji Kutumia Mitandao ya Kijamii” kuhusu jinsi orodha ya matangazo ya WhatsApp inavyoweza kutumika kushirikisha wasikilizaji wako. Kazi ya pekee ya msimamizi wa WhatsApp ni kutuma ujumbe kwa orodha na kuhakikisha kuwa sheria za usawa na usalama zinazingatiwa kila wakati vikundi vya WhatsApp vinatumika katika timu ya wanahabari vijana. Jukumu la msimamizi wa WhatsApp ni:

- Kuelewa udhibiti wa kikundi. Unaweza kuamua ikiwa washiriki wote au washiriki wa kikundi pekee ndio wanaweza kutuma ujumbe kwa kikundi. Kutumia ‘feature’ hii ya WhatsApp inaweza kusaidia kupunguza mazungumzo yasiyokuwa na maana au usumbufu wakati wa mahojiano au wa mwingiliano na mgeni wa kipindi
- Kutengeneza ujumbe mfupi wa kukaribisha washiriki: “Karibu kwenye kituo chetu cha WhatsApp” kinachoeleza kanuni za kikundi na ambacho kinaweza kutumika kila wakati unapoanzisha kikundi kipya au orodha mpya ya matangazo

Mwezeshaji wa Vijana: Mwezeshaji ndiye mshauri anayefanya kazi na kituo cha redio, vijana na ofisi za CRF/MYCN kuhakikisha kuwa kila wiki sauti za vijana husikika hewani. Jukumu la mwezeshaji ni:

- Kuhakikisha kuwa kanuni za usalama za kutoa taarifa tokea nyumbani zinazingatiwa kila mara kipindi kinapotengenezwa
- Kusaidia wanahabari vijana katika hatua zote za utengenezaji wa vipindi vyao vya redio
- Kuchanganya kipindi cha mwisho na kukipakia tayari kwa kurusha hewani
- Kuhifadhi vipindi vya redio na vipengele kwenye SoundCloud

KIKAO CHA MATAYARISHO YA KIPINDI TOKEA NYUMBANI

Sasa kwa kuwa unaelewa majukumu na kazi tofauti zinazotakiwa ili kutoa taarifa tokea nyumbani, unahitaji kufikiria jinsi ya kupanga vikao vinavyohitajika ili kuhakikisha kuwa kuna vipindi vya kurusha hewani.

Vikao vya utengenezaji wa vipindi vya kila wiki vinaweza kufanywa kwa upangaji wa ripoti tokea nyumbani. Inayohitajika tu ni kuamua jukwaa ambalo mtakutana. Tunawashauri mchague kati programu za bure zifuatazo:

- WhatsApp, ambayo inaweza kuwa na sehemu za video na watu 4 kwa wakati mmoja.
- Skype, ambayo inaweza kuwa na simu za sauti au video na hadi watu 50 kwa wakati mmoja.
- Zoom, ambayo inaweza kuwa na simu za video na hadi watu 100 kwa dakika 40.
- Houseparty, ambayo inaweza kuwa na simu za video na washiriki 8 kwa wakati mmoja.
- Google hangouts, ambayo inaweza kuwa na simu za video na watu 10 kwa wakati mmoja.



Vikao vya utayarishaji husimamiwa na mtayarishaji wa kipindi. Kama mtayarishaji, hakikisha kuna ajenda ya kila kikao ili usipoteze muda na data. Tunapendekeza kuzima video na utumie sauti tu katika vikao ili kupunguza gharama za data.

Kabla ya kuzindua kikao chako tokea nyumbani kwanza unatakiwa kutoa

taarifa na kutayarisha vipindi vya COVID-19, tunapendekeza kiwe kikao cha kwanza (kick-off meeting) na washiriki wa kundi lako ili muamue jinsi ambavyo vikao vya kutayarisha/kuandaa vipindi vinapaswa kuwa, kulingana na mitandao ambayo washiriki wa kundi wanaweza kutumia kiurahisi. Kikao kwanza ni kikao cha kupanga na kufafanua mikakati mtakayohitaji kuweka ili shughuli ziendelee vizuri. Baadhi ya mambo ambayo mnaweza kuzungumzia katika kikao chenu cha kwanza ni:

- Wakati mtakutana
- Mtakutana katika mtandao upi
- Ajenda ya kikao cha maandalizi/matayarisho ya kipindi zitakuwa zipi, yaani mtakacho jadili katika kila kikao na kwa utaratibu gani, kwa mfano:
 - Tafakari na mafunzo kutoka kwa matangazo ya hivi karibuni
 - Kuchagua mada na mada mahususi
 - Kuchagua majukumu na wajibu
 - Kupanga ratiba ya kipindi (show-clock)
 - Kutayarisha scripti/muongozo
 - Kuamua tarehe ya kuwasilisha vipengele vyote vya kipindi cha redio
- Mtakutana mara ngapi kama kundi zima na ni kikao gani zaidi kitahitajika, kwa mfano:
 - Vikao vya ziada ni vikao vinavyolenga eneo ambalo sio maalum kwa kila mtu. Baadhi ya vikao vya ziada ambavyo vinaweza kufanyika kando na mkutano wa kutayarisha kipindi kwa kila wiki inaweza kujumuisha:
 - Kikao cha watafit wa kipindi ilii waweze kushiriki taarifa zao na wanahabari na waweze kupata maoni kuhusu kile wameshaweza kufanya

na kurekodi tayari.

- Majadiliano ya kupanga scripti za kufungua na kufungua kipindi/kipengele

Hivi karibuni utaona kwamba kuripoti na kurusha vipindi tokea nyumbani kunahitaji kuwe na mipango madhubuti na mawasiliano mazuri! Njia moja ya kupanga ni kuaandaa mpango wa kila mwezi, badala ya kila wiki. Mipango ya mwezi hukuruhusu kutabiri mambo yajayo katika mwezi mzima ili uweze kuwa tayari. Baadhi ya mambo ambayo unapaswa kujumuisha katika mpango wako wa kila mwezi ni:

- Nyakati za mitihani
- Sikukuu
- Matukio ya kituo cha redio
- Wiki ambazo unaweza kucheza vipindi

vilivyorekodiwa vya mada zingine ambazo umeshughulikia, kwa mfano, elimu, mabadiliko ya tabia nchi, haki za afya ya jinsia na uzazi, nk.

- Ujumbe unaofaa kutoka kwa vyanzo vingine ambavyo vimetumika, kuongeza katika kipindi chako, kwa mfano, habari kutoka UNICEF au Wizara ya Afya.

KUTAFUTA WAGENI WA KIPINDI WAKATI UNAPOTOA TAARIFA TOKEA NYUMBANI

Unapataje wageni wa kipindi na utaalika nani kushiriki kwenye kipindi chako wakati harakati zako zimezuiliwa? Hii itakuhitaji utafute njia za ubunifu na kutazama rasilimali ulizo nazo tayari. Ukitafakari vipindi vyote vya redio na shughuli za kijamii ambazo umeandaa kwa miaka mingi, tayari umeshafanya kazi na safu kubwa ya wageni ambao unaweza kuwashirikisha.

Vidokezo kadhaa vya kupata wageni wa kipindi tokea nyumbani:

- Ongea na stesheni ya redio kuwauliza kama unaweza kupata wataalam wa karibu. Ikiwa stesheni ya redio ina uhusiano na watu kama wataalamu wa huduma ya afya, polisi, tabibu na viongozi wa dini, unaweza kuuliza stesheni ikuunganishe na wadau hao ambao wanaweza kuchangia mada.
- Wengine mmefanya majadiliano ya jamii na shughuli za kijamii. Angalia orodha ya usajili wa mahudhurio ya watu ambao umefanya kazi nao na ufutatlie kuhusika kwao katika janga la COVID-19. Orodhesha watu ambao unafikiri wanaweza kuwa wanahusika katika mapambano dhidi ya COVID kama wageni wanaoweza kutumika kwenye kipindi.

- Kuwa makini kwa kile watu wanachosema kwenye mitandao ya kijamii. Ikiwa kile mtu anasema ni cha kulisimua, chenye mawazo, cha kugusa moyo, au cha kuelimisha, basi anaweza akawa mgeni wa kipindi chako.

Unataka mgeni ambaye yuko tayari kusimulia hadithi yake, na ikiwezekana, kuisimulia vizuri. Wakati mwingine hisia zinazoletwa na mtu asiye mzungumzaji maalum wa umma, lakini anayeweza kutoa ushuhudia wake mwenyewe, zina nguvu zaidi kuliko hotuba ya mwanasiasa. Wahimize wageni kuzingatia mambo yale hufanya hadithi ziwe za kupendeza kwa wasikilizaji.

Viungo vya hadithi nzuri ni pamoja na:

- Mwanzo, katikati, na mwisho (ingawa sio kila wakati husimuliwa kwa utaratibu huu)
- Maelezo ya kina
- Hisia
- Sauti za kunogesha hadithi (sound effects)
- Kitendo au tuhuma
- Sauti halisia
- Mtiririko
- Matamshi



Kumbuka, wakati wa kuchagua wageni, awe mtu mwenye nguvu/ushawishi. Watu tunaopata habari kutoka kwao hawahitaji kuwa wataalam, lakini pia wanaweza kuwa watu wa kawaida wenye uzoefu wa kibinafsi unaohusiana na mada.

Mara tu utakapotambua mgenii wa kipindi chako cha COVID-19, chagua aina ya muundo wa redio unaofaa kuwasilisha hadithi yao.

3. KUTUMA TAARIFA KUTOKEA NYUMBANI

TAFSIRI

Hapo chini kuna ufafanuzi utakao kusaidia kuelewa misamiati kadhaa ambayo utakutana nayo katika sura hii.

Kutoa/kutuma taarifa kutokea nyumbani (remote reporting):

Tukizingatia kwamba kazi nyingi inazohusiana na wanahabari hufanyika uso kwa uso, janga hili linahitaji tutafute njia za kujiweka salama, huku tukiendelea kufanya kazi muhimu ya kutoa taarifa sahihi kwa umma. Kutoa taarifa kwa umbali kunatuhimiza tupate njia za ubunifu tukitumia rasilimali na teknolojia tuliyonayo nyumbani. Kwa wengi wetu, kutumia simu za mkononi za kisasa huchukua nafasi ya vinaso-sauti (rekoda) na ndio njia iliyo rahisi kwetu kurekodi na kutuma sauti zetu zirushwe hewani.

Simu ya mkononi ya kisasa/ simu mahiri (smartphone):

Simu ya mkononi ya kisasa ni simu ya rununu inayojumuisha kazi za hali ya juu, zaidi ya majukumu ambayo huturuhusu kupiga simu na kutuma ujumbe wa maandishi. Simu nyingi za kisasa zinaturuhusu kuchukua picha, kuingia

mtandaoni, kufanya utafiti wa mtandao na kurekodi sauti. Wakati wa janga la COVID-19, tunapoanza kuzoea kurekodi kutokea nyumbani, simu ya mkononi imekuwa kifaa kinachosimamia rekoda zetu za kawaida. Idadi ya bakteria inayopatikana kwenye simu ya mkononi kwa kawaida ni zaidi ya ile inayopatikana kwenye meza yako ya jikoni, kwenye kifunguzi cha mlango na hata kwenye kiti cha choo. Na ndio sababu ni muhimu sana kusafisha kifaa chako mara kwa mara kama unavyofanya mikono yako na maeneo mengine, ili kukomesha kuenea kwa COVID-19.

Kurekodi sauti:

Simu nyingi za mkononi za kisasa zina kifaa cha kunasa sauti katika orodha ya mpangilio au hata ndani ya WhatsApp. Kipaza sauti ni ishara ambayo hutumika sana kwa kutambulisha kifaa cha kurekodi sauti. Changamoto kuu kwa kutumia simu yako ya mkononi kama kinaso sauti ni kupata sauti kwa ufasaha. Kipaza sauti kilicho kwenye simu zetu za mkononi sio nzuri kama rekoda zetu, kwa hivyo tafadhali chukua fursa ya kufanya mazoezi kwenye kifaa chako ili upate ubora wa sauti unaowezekana.

KUJIFUNZA JINSI YA KUTUMIA SIMU YAKO YA MKONONI KAMA ZANA YA KUTOLEA TAARIFA

KUJIREKODI

Ili kutumia simu yako ya mkononi kama zana ya kuripoti, utahitaji kuelewa jinsi nyanja za kiteknolojia na ubora wa sauti ya simu ya mkononi hutofautiana na ubora wa sauti ya kinasa maalum. Kuna vitu ambavyo havibadiliki, na vingine ambavyo ni tofauti. Hivi vimeorodheshwa hapa chini:

- Wakati wa kutumia kinasa sauti, unavaa kifaa cha kusikiliza sauti (headphones/earphones) kila wakati ili kusikiliza ubora wa sauti wakati wa kurekodi.
- Kama unavyofanya kawaida unapotumia kinasa sauti, kila wakati anza kurekodi sekunde chache kabla ya kuzungumza kwenye simu yako, na uache sekunde chache baada ya kumaliza kuongea, kabla ya kubonyeza kitufe cha kusimamisha, ili kuhakikisha hautakata mwanzo au mwisho wa kurekodi kwako.
- Simu nyingi zina kinasa sauti (maikrofoni) katika sehemu ya chini ya simu, na vipokea sauti kando yake. Wakati wa kurekodi, hakikisha kwamba kipaza sauti cha simu kiko kwenye mwelekeo wa mdomo wako. Kuwa mwangalifu usifunike kipaza sauti na mkono wako wakati wa kurekodi.
- Tofauti na kinasa sauti ambacho unashika sentimita 10 (takribani ukubwa wa ngumi) mbali na mdomo wako, utahitaji kuweka kipaza sauti cha simu karibu 2 cm (urefu wa kidole chako cha gumba) mbali na mdomo wako wakati wa kurekodi. Hii ni kwa sababu maikrofoni ya simu haina nguvu kama kinasa sauti (rekoda). Basi ni muhimu kushikilia simu karibu na mdomo wako ili unase sauti yako vizuri.
- Tofauti na rekoda ambapo unaweza kubadilisha viwango vya kurekodi, simu hazina uwezo huo. Ukitumia simu yako, fanya mazoezi ya kujirekodi, ukipima viwango vya sauti kulingana na umbali wa simu hadi mdomo. Ikiwa simu iko karibu sana utachukua sauti za kelele za mdomoni (clicks na pops) na kupumua kwako pia, ambayo haitapendeza kwa wasikilizaji wako. Ikiwa tena simu iko mbali sana, sauti yako itakuwa laini sana na isiyoeleweka vizuri. Pima hii kwa kutumia viwango tofauti vya sauti, kutoka kwa sauti ndogo ya kunong'oneza (whisper) hadi kupaza sauti kubwa (shout). Programu zengine za simu, kwa mfano 'Sauti ya Memo' kwenye simu aina ya iPhone, inakuonyesha "mawimbi ya sauti" ambayo huja unapoongea, ikikupa kiashiria cha kama viwango vyako vya sauti viko juu au chini zaidi.
- Kabla ya kuanza kurekodi kwenye simu yako ya mkononi, zima kelele za kifaa hicho (mute) au uweke kwenye 'hali ya ndege' (airplane mode). Hii itazuia sauti za ujumbe au simu zinazoingia kuingilia.
- Hakikisha umepaza sauti yako ili usikike vizuri. Jipime mwendo kwa kuzungumza kwa kutumia sentensi fupi. Tunapotumia sentensi ndefu na ngumu, tuna tabia ya kujaza maneno mengi kwenye pumzi moja. Kuwa makini kwa kupumua kwako, pumzika wakati wa mahojiano/rekodi yako. Kugeuza kichwa chako pembeni na kila unapopumua kutaepuka kurekodi sauti nzito za kupumua ambazo zinahitaji kuhaririwa baadaye!

KUREKODI MAHOJIANO NA MTU AMBAYE HAYUKO CHUMBANI NAWE

KUNA NJIA TOFAUTI ZA KUKUSANYA SAUTI KUTOKA KWA MTU AMBAYE HAYUPO NDANI YA CHUMBA NAWE.

- Njia ilio rahisi kabiza, kutoka kwa maoni ya kiteknolojia, ni kuwatumia maswali mapema na kuwauliza watume majibu yao kwa ujumbe wa sauti wa WhatsApp au kurekodi sauti. Kanuni za kurekodi mahojiano kupitia ujumbe wa sauti.



- Kurekodi mahojiano moja kwa moja, unaweza kupiga simu ya mtu huyo, kuweka spika ya sauti kubwa na kutumia smartphone nyingine kurekodi. Ubora wa mahojiano unaweza kuwa mzuri kama notisi ya sauti, lakini bado itafanya kazi.
- Pia unaweza kutumia programu zinazopatikana bure, kama Anchor (anchor.fm) ambayo hukuruhusu kurekodi mahojiano ya simu, hata ikiwa mhojiwa wako hana programu hiyo kwenye simu yake.

MAZOEA BORA (MAPENDEKEZO) YA MATUMIZI YA WHATSAPP

WhatsApp ni programu rahisi kutumia inayopatikana bure na inayomilikiwa na kampuni ya Facebook. Inakuruhusu kutuma na kupokea ujumbe wa maandishi, simu za sauti na za video, picha, hati, pini za eneo na ujumbe wa sauti. WhatsApp ndio programu ya kwanza ya ujumbe katika bara la Afrika, na kipengele chake cha ujumbe wa sauti ni kizuri kwa shughuli za kuripoti tokea nyumbani. Hii ndio sababu kuu tunakuhimizai utumie WhatsApp pindi unaporekodi taarifa zako tokea nyumbani, lakini kwanza, tupate vidokezo vichache:

- Tumia na usimamie akaunti yako mwenyewe ya WhatsApp kwa mazungumzo ya moja kwa moja na kikundi kidogo: Kwa madhumuni ya usalama wako, patia wasimamizi wa WhatsApp katika kikundi chako jukumu la kuunda kikundi cha WhatsApp ambapo mazungumzo yote na wageni yatafanyika. Kundi hili la WhatsApp linapaswa kujumuisha mwezeshaji wako, msimamizi wa WhatsApp na wahusika wa kikundi chako. Futa na kuongeza wageni kama itakavyohitajika kwa kila kipindi. Ni muhimu umfanye mwezeshaji wako awe msimamizi mmoja katika vikundi vyote vya WhatsApp ili kuunda mawasiliano na wageni, na ili pia kuwe na uangalizi. Kumwingiza mwezeshaji wako katika vikundi vyote vya WhatsApp inaruhusu uangalizi, uwazi, uwajibikaji kwa jamii na utunzaji.
-  Unapaswa kupata ruhusa kutoka kwa wageni wa kipindi na washiriki wako kabla ya kuwaongeza kwenye kundi: Ikiwa utaongeza mtu kwenye kikundi na ajiondoe, tafadhali heshimu maamuzi yake na usimuongeze tena, isipokuwa akikuuliza umwongeze humo tena.
- Pata idhini ya watu: Ujumbe unapaswa kutumwa tu kwa watu ambao wamewasiliana nawe kwanza au ambao wamekukubalia kuwasiliana nao kupitia WhatsApp. Ni bora kuwapa watu chaguzi kulingana na aina ya mawasiliano wanayopendelea na kisha, unaweza kupendekeza WhatsApp, ukielezea vitendea kazi vyake ambavyo huifanya iwe vizuri kwa kufanyia kazi kutuma ripoti.
- Heshimu uchaguzi wa watu. Haijalishi uzuri wa simulizi yao : Ikiwa mgeni ambaye amehojiwa au ameishiriki hadithi yao kwa kutumia moja ya miundo, na kisha akaamua anataka atolowe kwenye kipindi, na kukuuliza ufute ujumbe wao, ni lazima uheshimu ombi lao. Ikiwa watakuuliza uache kuwatumia ujumbe, ondoa mgeni huyo kwenye kipindi kwa kumtoa katika kitabu chako cha anwani na usiwasiliane naye tena.
- Fikiria mara mbili kabla ya kusambaza ujumbe: Wageni wa kipindi wakipeana ridhaa ya hadithi na maoni kutangazwa hewani, haimaanishi kwamba wamekupa ruhusa ya kusambaza walichorekodi kwa wawasiliani wako. Usitumie wengine hadithi ambazo mgeni amerekodi na akakutumia.
- Kutumia orodha za mawasiliano ambazo sio zako: Usitoe kamwe namba za simu za wageni wako bila idhini yao.
- Orodha ya matangazo: Ujumbe uliotumwa kupitia orodha ya matangazo unaweza tu kupokewa wakati mtu amejumuisha maelezo yako ndanii ya orodha yake ya namba za simu.. Kumbuka kuwa utumiaji wa ujumbe wa matangazo unaweza kusababisha wasikilizaji kuripoti ujumbe wako. Tafadhali kumbuka kuwa WhatsApp inaweza kuzuia akaunti ambazo zimeripotwa kuwa zinatuma ujumbe nyingi zaidi.

KANUNI ZA KUREKODI MAHOJIANO KUPITIA UJUMBE WA SAUTI

Hapa kuna miongozo kwako, mwanahabari, ya wakati unafanya mahojiano kupitia ujumbe wa sauti, ambapo wewe na mhojiwa mnabadilishana ujumbe wa sauti ili kuzalisha mtiririko mzuri kama wa mahojiano ya moja kwa moja.



MIUNDO, Mahojiano

FANYA	USIFANYE
<p>Mpe mgeni maelezo wazi ya kile unachotafuta kwa kumuuliza swali zuri, au kuwa maalum, kuhusu aina ya hadithi au uzoefu ambao ungependa kusikia zaidi.</p>	<p>Usiogope kutoa ujumbe wa sauti ukiwa ni mrefu zaidi, au mgeni anaacha mada au kutoa matamshi yasioyofaa, lakini hakikisha umeifanya kwa njia yenye heshima.</p>
<p>Tambulisha wageni kwa jina na uwashukuru baada ya kutoa mchango wao.</p>	<p>Usitume maelezo ya sauti kutoka kwenye mahojiano kwa marafiki wako, haswa sehemu za kusisimua.</p>
<p>Tumia maswali ya wazi ili kuruhusu wanaohojiwa kufafanua na kuongeza habari zaidi, pamoja na hisia, mitazamo na uelewa wao wa mada hiyo.</p>	<p>Jaribu kutotumia maswali yaliyojifunga.</p>
<p>Mweleze mgeni kuhusu njia za kurekodi ujumbe wa sauti na mazingira bora ya kurekodia.</p>	<p>Usilazimike kuchukua ujumbe wa sauti ambao haufurahii. Eleza mgeni kwanini haiwezi kutumika na kisha umuombe aifanye tena.</p>
<p>Kuwa mkarimu na mwenye heshima na uruhusu wageni kuwa na maoni yao, hata ikiwa haukubaliani nayo.</p>	<p>Jaribu kutorekebisha koo, kupiga chafya au kukohoa ndani ya kipaza sauti. Jaribu kuweka unachorekodi kikiwa wazi iwezekanavyo.</p>

Sasa, hapa kuna miongozo kadhaa ya kuwapa wageni wa kipindi ili kuhakikisha wanarekodi sauti zao kwa ubora wa kutumika kwenye kipindi cha redio:

- Hakikisha kuwa uko kwenye chumba kilicho kimya.
- Weka simu yako karibu na mdomo wako, na usikilize ukitumia kifaa cha kuskilizia sauti (headphone) ili kuhakikisha ubora wa sauti.
- Changia papo hapo kwa mada ambayo imeandaliwa badala ya kupoteza muda na salamu nyingi na utangulizi mrefu.
- Kuwa wazi, na fikiria kwa kina kuhusu ujumbe unaojaribu kuwasilisha.
- Jua unachotaka kusema kabla ya kuanza kurekodi. Labda hata unaweza kuiandika

kwanza, lakini usiisome ili kuyatunza mazungumzo yawe ya kuisisimua

- Epuka kujirudia-rudia
- Zingatia urefu wa unachorekodi ili uendane sambamba na muda uliopangwa kulingana na muundo/kipengele.



Wajulishe haya wageni wako katika kila hatua ya mchakato. Kumbuka kuwa wageni wako sio wanahabari wa redio na hawatarekodi sauti zilizo tayari kwa redio kama unavyoweza.

MIONGOZO NA MAZINGIRA YA KUREKODI



- Rekodi wakati ambao hautarajii kupokea simu ili kuhakikisha usumbufu wa mlio wa simu kuingia hautatizi kurekodi kwako, au pia unaweza badilisha simu yako na kuiweka kwenye hali ya kimya ya usafiri wa ndege (airplane mode)
- Hakikisha kwamba betri yako ya simu ina angalau 80%.
- Hakikisha kuwa una nafasi ya kutosha kwenye simu yako ili kuhifadhi utakachorekodi.

Pindi unapozishika vizuri mbinu za kurekodi, ni muhimu pia kuzingatia mazingira ambayo unarekodia.

Kwa ubora wa hali ya juu, ni vizuri kila wakati kurekodi kwenye chumba kidogo chenye ukimya na utulivu, mahali ambapo unajua hakuna mtu atakayeingia na kukuvuruga. Ikiwa kuna pazia, zifunge, kwani itapunguza sauti ya mlio ambao unaweza kuingia katika vyumba vingi. Weka kila kitu unavyotaka kabla ya

kuanza kurekodi. Hakikisha umeangalia kelele zinazoweza kuingilia kati zinazotokana na vitu kama viyoyozi, taa za umeme, jokofu, trafiki, redio, au ufunguzi wa karatasi za pipi. Zima vifaa vya kelele au kaa mbali navyo. Tofauti na rekoda, maikrofoni ya simu haina nguvu sana, kwa hivyo ni vizuri ikiwa unaweza kurekodi katika mazingira tulivu.

Kuripoti kutafanywa tokea nyumbani, na kuna uwezekano kwamba utakutana na usumbufu kutoka kwa wanafamilia ambao mnatumia nao nafasi/sehemu moja. Ili kupunguza matatizo haya, unaweza:

- Kurekodi wakati unajua nyumba ni tulivu zaidi, kwa mfano wakati wanafamilia wamelala.
- Panga ratiba yako ya kurekodi na uwape familia taarifa ya mapema, ambao utaomba nafasi hiyo kuwa kimya.

Kelele za nyuma zinaweza kuchokoza na kugeuza usikivu wa wasikilizaji wako mbali na habari ambayo unawaandalia. Fikiria njia ambazo unaweza kupata usaidizi kutoka kwa watu wanaokuzunguka. Waeleze kuwa utakuwa unarekodi, na kuwa unawaomba kwa heshima watulie inapohitajika.



Unapaswa kuhakikisha kwamba mazingira ya kurekodi ya wageni wako yapo kimya isipokuwa kama ni ujumbe wa sauti uliorekodiwa katika eneo la tukio (on location)



Miundo

KUANDIKA ORODHA YA UNACHOREKODI

Unapotumia simu yako, ni muhimu kuandika unachorekodi kama vile tu unapofanya wakati unatumia kifaa cha kurekodia (digital recorder). Tayarisha maelezo sahihi na mfumo wako wa kuweka vitu katika hifadhi yako mwenyewe: kila kifaa cha kurekodia kinakuja na kitabu. Unaweza kutengeneza moja cha simu yako kwa kutumia daftari dogo au kutumia programu ya vidokezo ilio kwenye simu yako.

Mpangilio wa maandishi kwenye kitabu chako cha kunukulia/kutunzia kumbukumbu ulichorekodi kinapaswa kuwa na vichwa vifuatavyo:

Tarehe:

Mahojiano na mada:

Muda wa mahojiano:

Jina la mtu ambaye uliongea naye:

MIUNDO

Kwa miundo miwili ya kwanza, maswali unayouliza na jinsi unayaunda ni muhimu kwa kukusanya habari kamili, na pia kwa kuwatia moyo wahojiwa kujibu kwa kutumia maneno ya kuelezea, hisia na sauti halisia ili kuimarisha hadithi.



MAHOJIANO



Kama ilivyoielezwa hapo juu, unapofanya mahojiano, una nafasi ya kuwa na mtu wa kumhoji. . Mahojiano yanaweza kufanywa kwa kutumia maelezo ya sauti. Wewe na mhojiwa hubadilishana sauti, kwa kuuliza na kujibu, ili kuwe na mtiririko wa mahojiano kama yale ya moja kwa moja (ana kwa ana).



Miongozo ya maswali mazuri:

- Uliza maswali ambayo hayaruhusu majibu ya 'ndio' au 'hapana' tu. Ikiwa mhojiwa anajibu na ndiyo au hapana, kila wakati fuatilia swali lako kwa kumuuliza "kwanini".
- Sio lazima ung'ang'anie tu na maswali ambayo yalitayarishwa. Sikiliza taarifa ya kufurahisha na isiyotarajiwa na uulize maswali ya kufuatiliza toka kwa mhojiwa.
- Kuwa mwangalifu usiulize maswali ambayo tayari yamejibiwa.
- Tumia maswali yaliyo wazi. Epuka maswali ambayo yanaelekeza majibu fulani, kwa mfano: "kujijiri wakati wa kizuizi cha kutoka nje lazima iwe ngumu, sivyo?" Njia bora ya kuuliza swali hili itakuwa, "Unahisi vipi kujijiri katika nyakati hizi zisizo na uhakika?" au "Tuambie ni jinsi gani unahisi kujijiri katika nyakati hizi za shaka".
- Dumisha urahisi unapouliza msawali. Usiulize maswali mawili kwa wakati mmoja. Watu kawaida hujibu swali la pili na kusahau la kwanza.

Mahojiano ya kufana kwa kawaida hujumuisha utafiti wa kina na kupanga mahojiano mbeleni. Baadhi ya mipango inapaswa kujumuisha:

- Kuamua mada mahususi ya kipindi chako cha COVID-19.
- Kujua unachotaka kutoka kwa mahojiano yako, kwa mfano, ushauri wa wataalam au hadithi za kibinafsi.
- Kupata watu ambao wanajua kuhusu mada yako ya kipindi na wataweza kukupa taarifa unayotafuta.
- Kutafuta mengi kadiri uwezavyo kuhusu mtu utakaye mhoji kabla ya kuhojiana naye.
- Kuandika maswali ya kuuliza, ukikumbuka kuwa sio lazima ushikilie maswali hayo yote.
- Kujitambulisha kwa njia ya simu na lengo la mahojiano yako.
- Kuwa mkarimu na mwenye heshima wakati wote.
- Kuelezea kwamba mahojiano yatafanyika kupitia maelezo ya sauti ya WhatsApp kwa sababu za usalama, ili kuwalinda wote kutokana na uwezekano wa kuambukizwa.
- Kuuliza mhojiwa idhini yake ya kuhifadhi mahojiano kwenye simu yako.
- Kutoa maelezo kwamba utatumia mahojiano kwenye kipindi kamili ambacho kitarushwa katika tarehe yako ya utangazaji.
- Kuandaa tarehe na wakati maalum wa mahojiano ya sauti na mtu ambaye utamhoji.

Wakati wa mahojiano:

- Anza kwa kuangalia ubora wa mazingira ya kurekodi ya mhojiwa kwa kufanya jaribio fupi la haraka. Hii inaweza kufanywa kwa kuuliza swali la kawaida lisilohusiana na mahojiano.
- Fuata kwa kumuuliza mhojiwa ajitambulisha mwenyewe.
- Tangu mwanzo kabisa, jaribu kumfanya mhojiwa ahisi ametulia.
- Ongea na mhojiwa wako, usisome tu maswali kutoka kwenye orodha. Wajibika kwa kile anachosema na utunzaji wa dhati.
- Mpe mhojiwa nafasi ya kufikiria kabla ya kukutumia majibu yake ya sauti. Usikashirishwe na sehemu za kimya kifupi au ukimya .
- Mwishowe, mshukuru mhojiwa, na umalizie mazungumzo kwa kuwaambia ni lini wanaweza kutarajia kusikia mahojiano yakirushwa hewani.



Mahojiano yote hayapaswi kuwa zaidi ya dakika 5. Kila taarifa ya muhtasari wa sauti inapaswa kuwa sekunde 30 - 45.



SAUTI YA UMMA



Sauti ya umma ni maoni manne au matano mafupi ya sauti zilizokusanywa kutoka kwa wanajamii kuelezea maoni yao kuhusu mada. Ni njia nzuri ya kufungua kipindi wakati zikionyesha maoni na mawazo ya jamii kuhusu mada kama COVID-19. Pia ni muundo mzuri wa kupima maarifa na ufahamu wa wanajamii kuhusu mada fulani.



Sauti ya umma inaweza kuuliza wanajamii: Uelewa wako wa COVID-19 ni nini?



Maswali ya sauti za umma yanaweza kutumwa kwa kutumia orodha ya mawasiliano ya redio kwa kutumia orodha ya utangazaji (broadcast list), bora washiriki waelewe kuwa wanahitajika kujibu kwa kutuma sauti (voice note).

Vitu kadhaa vya kuzingatia hapa ni:

- Hakikisha umeweka muda wa mwisho wa kuzipokea ili upate majibu kwa wakati unaofaa ili uweze kuyajumuisha na kuyatuma kurushwa hewani.
- Wahimiza wanajamii kujibu kwa uaminifu. Bila kufikiria kuhusu swali zaidi au kwenda kufanya utafiti. Sio kuhusu kutoa jibu sahihi au kukosa, wala hakuna tuzo ya jibu sahihi, mbali tu ni njia ya kupima uelewa wa jamii.



Kipengele cha sauti ya umma kinatakiwa kisizidi dakika 3. Kila sauti ya umma inatakiwa kuwa na urefu wa sekunde 20-30



WASIFU WA SAUTI



Lengo la wasifu wa sauti

Wasifu wa sauti ni muundo bora wa kupata hadithi/simulizi, safari na uzoefu wa mtu ambaye ameathiriwa na mada inayoangaziwa katika kipindi chako. Wageni hawa sio wataalam kila wakati, lakini mara nyingi huwa ni watu wa kawaida wenye maoni ya maana. Muundo huu huruhusu ushiriki kwa kina na tafakari, na kutafakari michango kutoka mitazamo tofauti. Wasifu wa sauti huwapeleka wasikilizaji katika safari ya kuhamasisha.



Mgeni kijana wa kike/kiume ambaye ameanza maabara ya mapafu ambayo inatumiwa kugundua COVID-19 katika sampuli.



- Sehemu ya 1 (mwanzo):
 - Muulize ajitambulisha na kukuambia kidogo kuhusu malezi yake (umri, shule na hali ya familia).
 - Muulize akuambie jinsi, lini na kwa nini alianzisha maabara ya mapafu.
- Sehemu ya 2 (katikati):
 - Muulize aeleze wakati maalum kwake au ni jinsi alivyojua kuwa alikuwa akifanya jambo sahihi
 - Muulize aeleze alivyohisi wakati mlipuko wa ugojwa ulipofika nchini mwake

na maabara yake ikachaguliwa kupima sampuli za virusi.

- Sehemu ya 3 (mwisho):
 - Muombe atoe ujumbe wa kuwatia moyo wasikilizaji na vijana wanaotamani kufanya kazi katika sekta ya matibabu.

Maswali kadhaa ya kuandalia wageni wako ili kuwasaidia kupanga muundo wao wa sauti:

- Naomba utueleze kuhusu wewe tafadhali?
- Unaweza kuelezea jinsi ulivyoanza kufanya hivi?
- Unaweza kuelezea wakati (au uzoefu) ambao hautasahau?
- Kufanya hivi hukupa nini haswa?
- Una ushauri wowote (au kutia moyo) kwa mtu ambaye anataka kufanya hivyo?



Wasifu wa sauti unapaswa kuwa na urefu wa dakika 2 - 3.



MAONI YA SAUTI



Lengo la Maoni ya Sauti

Maoni ya sauti hutuletea maoni kutoka kwa mtu ambaye anaweza kuwa karibu au mbali na mada yako. Uhusiano wao na mada hio hata ukiwa ni upi, wanaonyesha kuwaza katika maoni yao na kutoa suluhisho zinazoonekana kwa suala hilo.



Daktari kijana ambaye hufanya kazi muda wa ziada katika moja ya hosiptali za karantini za COVID-19. Yeye hufanya kazi ya ziada kusaidia wakati wa mlipiko huu na anaamini raia wenzake wanapaswa kufuata sheria za kujitenga na kukaa nyumbani kwao.



- Sehemu ya 1 (mwanzo):
 - Anatoa taarifa kuhusu suala linalofuatwa na maoni yake. .kwa mfano: Nakubali kuwa raia wenzangu wanapaswa kufuata sheria za kujitenga wakati wa mlipuko wa COVID-19 ...
 - Yeye anafuata hii na utangulizi, akijitambulisha.
- Sehemu ya 2 (katikati):
 - Anaendelea kutoa maoni yake. Anaendeleza hoja yake, na kutumia mifano ya kibinafsi na / au anatoa ukweli na takwimu zinazounga mkono maoni yake.
- Sehemu ya 3 (mwisho)
 - Anamaliza kwa sentensi yenye nguvu na ambayo inatoa suluhisho ambalo ni la uhakika.



Maoni ya sauti yanapaswa kuwa na urefu wa dakika 1 - 2.



TAARIFA ITOKAYO MAHALI KWENYE TUKIO (ON LOCATION)



Lengo la taarifa tokea kwenye tukio

Kwenye sauti (voice note) ya eneo ni muundo ambao wanajamiii wanaelezea tukio la moja kwa moja au uzoefu. Wanajamii wanaweza kutuma ujumbe wa sauti kutoka kwa eneo la tukio lililopangwa kuwa la habari, kama vile: maelezo mafupi ya rais kuhusu COVID-19, au ujumbe wa sauti kutoka hospitali ambayo wagonjwa wametengwa. Ujumbe wa sauti unaodokeza habari zinaweza pia kujumuishwa wakati wanajamiii wanaripoti kutoka katika tukio ambalo jambo limetokea, kama wanahabari raia (citizen journalists), kama vile kuripoti kuhusu tukio haramu wakati wa karantini ya kukomesha kuenea kwa maambukizi au wakati huduma za jeshi hufika ili kudhibiti harakati katika jamii.



Maelezo ya sauti yanayotoka eneo la tukio huvutia na kufurahisha wasikilizaji kuyasikia, lakini ikiwa yanaweka mtu ambaye anayarekodi katika hali ya hatari ya kupata maambukizi ya virusi, kushambuliwa au kukamatwa, basi anapaswa asiyarekodi. Ni muhimu kutanguliza usalama wako mwenyewe na wa wengine wakati wote.



Waandishi wa habari na wanahabari raia wanapaswa kufuata mwongozo ulio hapa chini wakati wa kurekodi kutoka kwenye maeneo ya matukio (on location):

- Utangulizi: wajitambulisha na waseme wakati na tukio.
- Maelezo: waeleza kile wanachoona kikiendelea kwenye hafla.
- Habari ya msingi: mwanajamii anafafanua kinachotokea, ni muda gani unaendelea, na habari nyingine yoyote muhimu.



Inahitaji utafiti kupata mtu wa jamii anayeweza kuwapa wasikilizaji historia au hadithi/simulizi ya msingi wa tukio. Mwanajamii huyo atahitaji kuhojiana na msimamizi au mratibu wa hafla na achukue yale aliyoyapata na kuyatafsiri kwa maneno yake wenyewe.

- Mahojiano: mwanajamii apate mtu katika hafla ili kujibu maswali kadhaa yaliyoandaliwa na ambayo wanaweza kuangazia kuhusu uzoefu wao wa hafla hiyo au kwanini waliamua kuhudhuria.
- Hitimisho: mwanajamii anafunga habari yote aliyoshirikishwa na kurudisha usukani kwa aliye studio/mtangazaji.

Vipengele vya kujumuishwa katika taarifa ya kutoka 'kwenye eneo la tukio (on location)' inapowezekana:

- Sauti ya kikawaida ya eneo (au tukio) hilo
- Mahojiano na mratibu
- Mahojiano na watu kwenye hafla hiyo
- Mwanajamii akielezea kile kinachotokea
- Mwanajamii akitoa habari kuhusu tukio hilo



Taarifa kutoka kwenye eneo la tukio inapaswa kuwa na urefu wa dakika 2 - 3.



UTUNZAJI SAUTI (AUDIO DIARIES)



Utunzaji au 'diary' ya sauti ni uwekaji kumbukumbu ya mawazo ya kibinafsi, mawazo na maoni kwa kutumia rekodi ya sauti. Ni njia rahisi ya kushika na kuelezea maoni na hisia. 'Utunzaji wa sauti hurekodiwa mara kwa mara/kila siku kwa kipindi cha muda fulani, kama tu vile mtu angeandika katika daftari. Njia hii ya uhifadhi mawazo ndio hufanya utunzaji wa sauti kuwa muundo wa binafsi, ambapo msikilizaji anapata kusikia kuhusu nyakati muhimu, mawazo na hisia za mtu anayerekodi.

Maingizo yanaweza kutofautiana kwa urefu na aina (yanaweza kuwa mazito, ya kufurahisha, yenye kupendeza au ya kusikitisha). Yanaweza kuchukua muundo wa shairi au wimbo. Yanaweza kuwa yameandikwa awali au kutungwa hapohapo. Ni muhimu kuzingatia yafuatayo kabla ya kuanza kurekodi:

- Amua ni ujumbe upi muhimu/hisia ambayo unataka kufikisha siku hiyo, zinazohusiana na mtazamo wako wa hali ya COVID-19.
- Ikiwa uliongea kuhusu kitu muhimu katika ingizo lako la mwisho na kuacha vitu hewani bila kuvimalizia vizuri, rejea nyuma kwenye kile ulichokuwa unazungumzia hapo awali, na ueleze jinsi hali ilivyotoke au kutotokea .
- Fikiria sauti za eneo ili kuboresha unaperekodi. Kelele za nyuma, kwa mafano, mgurumo kama ile ambayo feni (ikitoa hewa) hutoa inaweza kuvuruga wasikilizaji, lakini ikiwa diary yako ya sauti inazungumzia utunzaji wa watoto wakati wa kukomesha kuenea kwa ugonjwa (lockdown), basi sauti za nyuma za watoto zinaweza kuongeza hisia za hadithi/simulizi hiyo.



Maingizo katika utunzaji kumbukumbu kila siku ya kijana anayeelezea maisha yake yalivyo katika hali ya kufungiwa nyumbani ili kukomesha kuenea kwa mlipuko wa ungonjwa yanaweza kuwa kuhusu kitu chochote anachopitia. Anaweza kuwa na wasiwasi kuhusu lini atakavyoweza kurudi shuleni, akipambana na nguvu za uhusiano na ndugu zake ndani ya nyumba, akiwa na wasiwasi kwa mama yao ambaye ni muuguzi katika hospitali ya umma, au hata kukariri tu jinsi ilivyo kufanya safari ya kila wiki kwenda dukani/sokoni au kile kinachotokea katika mitaa ya kitongoji chake.



Hifadhi za sauti zinapaswa kuwa za urefu wa dakika 2-3.

JE, WAJUA?

Muundo wa 'Je, wajua' inatumika kuorodhesha na kutoa ukweli wa kufurahisha, na taarifa rahisi na zenye ujuzi. Hizi zinaweza kutolewa kwa njia ya takwimu, namba na taarifa.



Je, wajua kuwa nchi ya St. Vincent na Grenadines ina idadi ya chini ya kesi za COVID-19, ikiwa na kesi moja tu iliyothibitishwa?

Huu ni muundo mzuri wa kufunga kipindi, kusisitiza ujumbe wa msingi wa mada na kuwajulisha wasikilizaji kuhusu ukweli uliowasishwa na kuthibitishwa unaohusiana na mada inayojadiliwa. Ina lengo la kufanya watu wadadisi na kutafakari kuhusu mada baada ya kipindi.

Hakikisha kuwa ukweli unaotoa ni mfupi na rahisi. Kauli ndefu zinaweza kusahaulika kwa urahisi na wasikilizaji.

Angalia na kudhibitisha ukweli wako kwenye vyanzo kadhaa, ili uhakikishe kuwa ukweli unaotoa uko sahili 100%.

Msimamizi wa kipindi atalazimika kufanya utafiti wa ukweli wa kuandaa katika kipengele cha 'je, wajua' unaohusiana na mada kabla ya kipindi, na kuongeza ukweli kwenye muongozo ili waweze kutoa ukweli kabla ya kumaliza kipindi.



Unaweza kusema kitu chochote cha ukweli kuanzia kimoja hadi vitatu kwenye sehemu ya "je, wajua".

KUFUNGUA NA KUFUNGA MIUNDO

Kwa sababu hauko hewani mwenyewe, mwanahabari anayerekodi muundo atahitaji kurekodi ufunguzi na ufungaji wa miundo yao. Hii itakuwa muhimu, haswa wakati kila sehemu itaunganishwa, na kukuruhusu kushika wasikilizaji wako mkono na kuwasafirisha nawe wanaposikiliza hadithi/simulizi za wanajamii na kupata uelewa mzuri wa mada.

Hapa kuna maoni kadhaa kuhusu jinsi ya kurekodi ufunguzi na ufungaji wa muundo wako:

- Hakikisha kwamba ufunguzi na ufungaji wa muundo inarekodiwa kama kanda tofauti kwa muundo wa sauti. Hii itaruhusu mabadiliko wakati wa mchakato wa uhariri.
- Fanya zote, ufunguzi na ufungaji wa muundo, zikiwa fupi
- Usieleze kila kitu. Toa habari za kutosha ili tu kushawishi/kuvutia wasikilizaji wako na uwape maelezo ya kutosha kwa ajili ya kujiunga na eneo la tukio na muktadha.
- Toa mawazo halisi ya katika ufungaji wako kwa kujibu muundo uliochezwa,

kufafanua kuhusu mambo yalioletajwa au sahihisha habari yoyote isiyo sahihi ambayo inaweza kuwa ilitolewa.

- Kaa mbali na misamiati ya redio siyoeleweka kwa urahisi na utumie tu lugha ambayo wasikilizaji wako wanaelewa



Njia ya kufungua kipengele cha sauti za umma sio “... kinachofuata ni sauti za umma kuhusu COVID-19”, lakini unaweza kusema kitu kama “Kinachofuata ni kuskiliza mtazamo wa jamii kuhusu COVID-19”.

- Hakikisha kuwa sauti yako inavutia wasikilizaji wako kukuskiliza. Jaribu kukuza ile nishati ambayo sauti yako ingebeba kama ungelikuwa unawasilisha kipindi chako cha redio moja kwa moja.

USHIRIKISHAJI WASIKILIZAJI KUPITIA MITANDAO YA KIJAMII

Changamoto moja kubwa ya kurusha kipindi kilichorekodiwa ni kwamba unapoteza uwezo wa kubadilishana mawazo na wasikilizaji wako papo kwa hapo. Sehemu hii inafungua njia ambazo tunaweza kuendeleza kubadilishana kati ya msikilizaji-na-mwanahabari, kwa kutafuta fursa ambazo mitandao ya kijamii inashikilia kwa kuziba pengo hili.

Ingawa utayarishaji wa vipindi kwa kurusha hewani utasimamiwa mapema, ushiriki wa wasikilizaji bado unawezekana kwa kutumia majukwaa ya mitandao ya kijamii kama Facebook, Instagram na hata WhatsApp

kupitia orodha ya utangazaji (broadcast list). Kumbuka kuwa wakati wa kipindi cha kawaida cha moja kwa moja, unatoa wito kwa wasikilizaji wapige simu kwa sababu tofauti. Wakati mwingine utahitaji wapige simu ili kujibu maswali ya wasikilizaji, nyakati zingine, kufanya majaribio au kusikia maoni tofauti kutoka kwa wasikilizaji wako. Na vipindi vilivyorekodiwa, shughuli hizi zitahitajika kuelekezwa kwa Facebook, WhatsApp au jukwaa lengine lolote la mitandao ya kijamii ambalo litakufaa zaidi. Ushirikiano huu pia unaweza kufanyika wakati wowote wa mchakato wa utengenezaji wa kipindi,

kumaanisha kwamba unaweza kujihusisha na wasikilizaji kabla, wakati huo wa kurusha hewani, na baada ya kipindi.

Ushiriki wa wasikilizaji kwa kutumia mitandao ya kijamii utahitaji majukwaa madhubuti ya mitandao ya kijamii. Utalazimika kuweka taarifa mpya katika jukwaa la mtandao wa kijamii kila wakati ili kuwafikia wasikilizaji vijana na watu wazima, ikiwa unataka wasikilizaji wakutambue kama jukwaa la mtandao wa kijamii wenye nyenzo za kujumlisha taarifa na habari, na kuwapa nafasi ambayo wanaweza kusikia vijana wakisema vitu vya kupendeza kuhusu janga lililopo.

Hapo chini kuna njia kadhaa za kushirikisha wasikilizaji wako kwa kutumia mitandao ya kijamii:

- Waulize wasikilizaji wako swali na kisha

uwaelekeze kwenye ukurasa wako wa Facebook kwa majadiliano hayo

- Uliza wasikilizaji washiriki majibu na maoni yao kupitia kwenye ukurasa wa Facebook
- Weka viunganishi (links) muhimu kwenye ukurasa wako wa Facebook kwa wasikilizaji ambao wangependa kujua zaidi kuhusu mada ya kipindi chako
- Weka taarifa mpya mara kwa mara ili wasikilizaji wako wazoe kuangalia ukurasa wako wa Facebook
- Fanya liwe jukwaa la kuaminika na linalowekewa taarifa mpya mara kwa mara, na kufanya watu kufuatilia kila mara.
- Jibu kila mtu. Futa maoni yanayodhalilisha na ufungie walio wasumbufu (trolls)
- Andaa mashindano na tuzo
- Tuma jaribio

JARIBIO (QUIZ)

Jaribio ni njia nzuri ya kupima kama wasikilizaji wameelewa dhana ambayo umetoa na kuifafanua katika kipindi chako. Fanya jaribio liwe rahisi na fupi na swali moja au mawili kwa kila kipindi.

Kwa kuwa kipindi chako kimerekodiwa tayari, itabidi uwaelekeze wasikilizaji kwenye kurasa unazopenda za mitandao ya kijamii au programu za kutuma ujumbe ili waweze kushiriki kwenye jaribio. Unaweza kutumia jaribio mara kwa mara iwezekanavyo, ili wasikilizaji wazoe kwenda kwenye kurasa zako za mitandao ya kijamii kila wanaposikiliza kipindi chako.

Swali zuri la jaribio unaloweza kuuliza wasikilizaji:

- Toa tafsiri (ufafanuzi) wa neno fulani gumu
- Toa tarehe muhimu ambayo ilitajwa kwenye kipindi
- Tambua mahali palipotajwa kwenye kipindi

Mawazo kadhaa ambayo husaidia kuendeleza jaribio vizuri:

- Zindua jaribio katikati au mwisho wa kipindi
- Toa tuzo kila wiki au tuzo kubwa mwishoni mwa mwezi kwa watu waliojibu maswali ya jaribio sahihi
- Toa taarifa muhimu na ukweli katika sehemu ya muundo wa 'je, wajua' au kama sehemu ya mazungumzo yako ya redio
- Ni muhimu kuhakikisha kwamba umetoa taarifa muhimu na wasikilizaji zaidi ya mara moja kwenye kipindi kabla ya kuzindua jaribio. Kwa njia hii, wasikilizaji walio makini wana nafasi nzuri ya kushinda.
- Usifanye maswali yako yawe magumu kwani hiyo inaweza kukatisha tamaa ya msikilizaji. Kumbuka lengo la jaribio ni kupima uelewa wa wasikilizaji wa kipindi, sio mtihani ambao wanahitaji kupita au kuanguka.

KUJIBU MASWALI YA WASIKILIZAJI WA KIPINDI

Kwa kuwa vipindi vya COVID-19 vitakuwa vimerekodiwa tayari, ushiriki wa wasikilizaji hewani utakuwa umezuiliwa kiasi. Kama ilivyoelezwa, moja ya njia za kuendelea kushirikisha wasikilizaji wako ni kwa kuwaelekeza kwenye ukurasa wako wa Facebook au orodha yako ya utangazaji ya WhatsApp (Broadcast list).

Hapa kuna miongozo kadhaa ya jinsi ya kuingiliana na wasikilizaji kutumia mitandao ya kijamii. Tutaangazia haswa orodha za utangazaji za WhatsApp (Broadcast list) na Facebook.

Hizi ni hatua unazopaswa kufuata ili kuweza kuandaa utangazaji wa moja kwa moja kutoka Facebook (Facebook live-stream) ili kushirikisha wasikilizaji:

- Nenda kwenye ukurasa wa kituo chako cha redio au ukurasa wa kikundi cha wanahabari vijana wa Facebook
- Juu ya sehemu ya habari (news feed) kwenye ukurasa wako wa Facebook, chini ya “tengeneza (create)”, chagua “moja kwa moja (live)” kwenye ishara ya kamera ya video (camcoder icon).
- Utaombwa utoe idhini kwa Facebook ili kufikia (access) kamera yako na kipaza sauti.
- Andika maelezo ya video ya kuvutia, ambayo yatafanya watazamaji watake kushiriki na kutazama video yako. Unaweza kuongeza eneo lako, tumia katooni za emoji, na pia kuwaalika watu (tag).
- Chagua mpangilio wa faragha kwa kubonyeza alama iliyopo kwenye kona ya mkono wa kulia wa chini na ufungue ‘vikwazo vya watazamaji’. Ikiwa kipindi chako cha redio kinatumia kurasa za kibiashara za Facebook, video yako ya moja kwa moja ya Facebook itakuwa wazi kwa umma.
- Kama kanuni ya jumla, epuka kuongeza mapambo kama kuchuja, lensi, au

michoro (doodle) yoyote kwa sababu itavuta mawazo ya watazamaji mbali na yaliyomo kwenye video yako, ambapo sio vizuri wakati wa kujadili mada muhimu kama COVID-19.

- Hakikisha kamera yako imewekwa kwa njia sahihi na kwamba nawe uko mahali sahihi kabla ya kubonyeza kitufe cha kuanza video moja kwa moja (start live video). Mara tu ukibonyeza kitufe hicho, video yako itaonekana kwenye sehemu ya habari (news feed) kwako, na kwa ya wasikilizaji wako pia. Kwenye kona ya kushoto ya juu, utaweza kuona muda video yako imekuwa ikiendelea.
- Wasiliana na watazamaji wako katika matangazo hayo ya moja kwa moja. Kumbuka, kwa sababu kipindi cha redio tayari kimerekodiwa, video hizi za moja kwa moja ndio njia pekee ambayo tunaweza kushirikishana na wasikilizaji wetu kwa wakati halisi, kwa hivyo jibu maswali na maoni yao wakati uko kwenye video ya moja kwa moja. Unapomaliza kurusha kipindi moja kwa moja, bonyeza kitufe cha “kumaliza” hapo chini kwenye kona ya mkono wa kulia. Baada ya hapo, unaweza kuchapisha video kwa ukurasa wako kutazamwa.



Matangazo ya moja kwa moja ya Facebook yanaweza kuendelea kwa muda wa hadi dakika 90. Lakini, kwa sababu wasikilizaji wako tayari wameshasikiliza kipindi chako, jaribu kuweka matangazo ya moja kwa moja yawe mafupi iwezekanavyo, bila kuzidisha urefu wa dakika 10. Kumbuka matangazo ya moja kwa moja ni ya kuwafanya wasikilizaji wako wahisi kuunganishwa na kipindi chako cha redio.

Vidokezo kadhaa vya kutengeneza video za kuvutia za moja kwa moja kupitia Facebook:

- Kuwa na muongozo wa kufungua na kufunga kipindi
- Fuata mbinu kama zile za redioni katika uandikaji na uipe mtiririko sawa na kipindi chako hewani
- Hakikisha kuwa maandalizi yako ya matagazo ya moja kwa moja yanafanyika mara baada ya kipindi cha redio, wakati bado kipindi chako kiko katika akili za wasikilizaji
- Hakikisha umefanya utafiti wa mada ya kipindi ili uweze kujibu maswali ya wasikilizaji.
- Kuwa na karatasi yako ya muongozo wa redio yenye maelezo kamili tayari kukusaidia
- Ingiza jaribio kulingana na sehemu ya “je, wajua?” ilioandaliwa katika kipindi.

Jinsi ya kujihusisha na wasikilizaji wako kwa kutumia orodha za kurusha matangazo ya WhatsApp:

Orodha ya matangazo ya WhatsApp ni sehemu muhimu ya kutoa habari na kikundi kikubwa cha wasikilizaji mara moja au pia kupata habari kutoka kwao. Orodha ya matangazo ya WhatsApp huruhusu hadi washiriki 256. Tafadhali kumbuka: njia pekee ambayo wasikilizaji wanaweza kutoka kwenye orodha ya matangazo ni ikiwa watafuta mawasiliano ya msimamizi (administrator) kutoka kwenye orodha ya namba katika simu zao, ambayo itazuia ujumbe wowote zaidi kuwafikia.

Njia zingine za kutumia orodha za matangazo ya WhatsApp ni pamoja na:

- Kusambaza matangazo ya jamii, habari, na maudhui mengine na wasikilizaji
- Kulenga vikundi maalum vya wasikilizaji na kura za maoni au jaribio, kwa mfano wasikilizaji wa watu wazima, vijana au

wasikilizaji ambao wanaweza kuwa wanafanya kazi katika tasnia fulani unayolenga

- Kutuma taarifa za kila wiki kuhusu mada ya kipindi kinachokuja na kuonyesha fursa zinazotokea
- Baada ya kipindi, kuwajulisha wasikilizaji wako kuhusu rasilimali katika jamii yako na viungo muhimu kwa kupata taarifa zaidi, nambari za msaada, tovuti na habari kuhusu mashirika ambayo watu wanaweza kutaka kuwasiliana nayo.

Msimamizi wa WhatsApp kwenye timu yako anahitaji kuongeza nambari za simu za wasikilizaji kwenye orodha yake ya namba za simu na kisha awaongoze kwenye orodha ya matangazo ya WhatsApp. Ni muhimu kutambua kwamba wasikilizaji watahitaji pia kuongeza nambari ya msimamizi kwenye orodha ya simu zao ili waweze kupokea ujumbe ambao umetumwa kutoka kupitia orodha ya matangazo. Ikiwa wasikilizaji hawataongeza nambari ya msimamizi, hawataupokea ujumbe uliotumwa kutoka kwa orodha ya matangazo.

Unapaswa pia kutuma kiunga cha SoundCloud kwenye kipindi chako kilichorekodiwa kwenye kurasa zako za mitandao ya kijamii. Kwa njia hiyo, washiriki ambao walikosa kipindi wataweza kupata fursa ya kukisikiliza kwenye SoundCloud.



Kuhifadhi vipindi/SoundCloud: angalia ‘Jinsi ya’ ili upate maelezo kuhusu jinsi ya kuhifadhi kipindi chako kilichorekodiwa kwenye SoundCloud.

KUTAFUTA MADA MAHUSUSI KWA KUTUMIA MITANDAO YA KIJAMII

Kadiri uelewa wa ulimwengu kuhusu COVID-19 unavyoendelea, ndivyo mazungumzo ya redio ya jamii utakayokuwa nayo yatabadilika. Wakati unapoenda, unaweza kugundua kuwa umebadilisha kipaumbele chako kutoka kwa kuwajulisha wasikilizaji wako kuhusu hatua za kinga, na kuanza kuangazia mazungumzo magumu zaidi ya unyanyapaa. Ili kipindi chako kiwe cha kufaa na ambacho watu wanadhamini, ni muhimu kuweka mazungumzo ya COVID-19 sanjari na mazungumzo ambayo yanaendelea katika jamii yako.



Tunajua kuwa janga hili litakuwa na athari hasi kwa uchumi wetu, lakini kuandaa kipindi kinachoangazia suala hilo haitakuwa na ubora kwa sasa, kwa sababu kile cha msingi na cha haraka katika hatua hii tulipo sasa ni habari za kujizuia na kukomesha kuenea kwa maambukizo mapya.

Mara tutakapohama kutoka katika awamu hii ya kwanza, na tumeelimika zaidi na ujuzi wa kudhibiti janga hili, mazungumzo ya COVID-19 yanaweza kuchukua mtazamo wa kitaifa. Huu ndio wakati ambapo hadithi za kibinafsi na athari zilizopata jamii tofauti kama matokeo ya janga hili yatakua. Mahali pazuri pa kupata hadithi/simulizi hizi za binafsi ni kwenye mitandao ya kijamii.

Watu hutumia mitandao ya kijamii kwa njia tofauti. Watu wengine huchapisha kila wazo lao, wengine huitumia kama njia ya kuhifadhi mawazo yao au kutoa tafakari zao za kibinafsi. Wengine huandaa kumbukumbu za uzoefu wao wa kubadilisha maisha au kutoa maoni yao kuhusu hafla za matukio na majadiliano. Haijalishi jinsi watu wanavyoshiriki,

mitandao ya kijamii itakuwa jukwaa nzuri la kupata mada mahususi za hadithi za COVID-19 kwa sababu ni nafasi ambayo inaweza kukuunganisha na watu walio nje ya mitandao yako ya kibinafsi, na watu wenye maoni na mitazamo tofauti.



Hata ingawa mitandao ya kijamii ni muhimu katika kupata mada mahususi mpya na taarifa, hakikisha umefanya utafiti wa mada hiyo kutoka kwenye vyanzo vingine vitatu tofauti (kwa mfano gazeti, tovuti ya kuaminika na makala iliyoandikwa na wataalam) ambayo inazungumza kuhusu mada hiyo hiyo. Hii itakuruhusu kupata mitazamo tofauti.

- Mitandao ya kijamii inaweza kukutanisha na watu zaidi kupita mitandao yako binafsi na kukuandalia maoni na mitazamo mipya. Ni jukumu lako kuhakikisha kuwa mada yako ya kipindi inafaa na inatumikia jamii yako. Unapochagua mada mahususi ya kipindi chako, jiulize maswali yafuatayo ili kuhakikisha kuwa mada uliyoichagua ni sawa kwa wasikilizaji kutoka katika jamii yako:
 - Unaweza kupata wahojiwa na vyanzo vya taarifa hiyo unayotoa?
 - Wasikilizaji wako watajali mada hii?
 - Hii ni mpya, muhimu au ya kupendeza kwa washiriki i wako?



Mara unapoamua mada ya kipindi chako, itangaze kwenye majukwaa yako ya mitandao ya kijamii ili kuwezesha washiriki wako kusikiliza kipindi chako cha redio.

KUDHIBITISHA UKWELI WA TAARIFA

Kumbuka kuwa kuripoti kutoka nyumbani kunakuhitaji ufanye utafiti wako zaidi mtandaoni, kwa hivyo hakikisha kukagua vizuri taarifa ambazo unasikia kutoka kwa wageni unaochagua kuwahoji, na habari unayopata mtandaoni. Sio habari zote tunazopata mtandaoni ni za kweli au sahihi, kwa hivyo ni jukumu lako kudhibitisha ukweli. Kuna habari nyingi bandia na habari za uwongo zinaenezwa kuhusu COVID-19, na kueneza habari ambazo sio kweli inaweza kuwa hatari. Kabla ya kutoa taarifa yoyote, hakikisha umeshaufanya uchunguzi wako wa kudhibitisha ukweli. Ili kudhibitisha ukweli wako kuhusu COVID-19, tumia tovuti za habari rasmi zilizopitishwa kama vile Shirika la Afya Duniani (WHO) au Vituo vya Udhidhi wa Magonjwa katika mkoa wako.

4. MAANDALIZI YA VIPINDI BAADA YA KUREKODI NA KURUSHA VIPINDI UKIWA NYUMBANI

VIPENGELE VYA KIPINDI CHA REDIO NA UHIFADHI

Ili mwezeshaji na timu ya CRF/MYCN waweze kutengeneza mchanganyiko wa mwisho wa kipindi na kupakia yaliyomo kwa wasikilizaji wako, watahitaji kupokea vipengele vyote pamoja, yaani 'box la zana za redio (Radio show kit)' kutoka kwako. Hilo box la zana limeundwa na vitu vifuatavyo: miundo ya redio, kipindi, na sauti za kufungua na kufunga miundo ya ndani na 'show clock'. Mwezeshaji wa CRF/MYCN watahitaji kuhariri kipindi cha redio cha dakika 30- 60 pamoja. Hapa chini kuna orodha ya vitu vya 'box la zana ' lako la redio ambavyo linapaswa kujumuishwa kila wiki:

- Ratiba ya kipindi ilioonyeshwa kwa saa (show clock)

'Show clock' ni ratiba ya kipindi ilioonyeshwa kwa saa, hatua kwa hatua katika mwongozo wa kipindi chako. Huu ni

mwongozo ambao mwezeshaji na timu ya CRF/MYCN watatumia kuhariri kipindi chako. Show clock itasaidia mwezeshaji na timu ya CRF kutoa kipindi ulivyokitazamia kuwa na kuhakikisha kwamba ni vile ulivyotaka kiandaliwe. Hii ni muhimu kwa sababu hata ikiwa unaripoti tokea nyumbani, vipindi vya redio vinahitaji kuwa vimetengenezwa na kijana, kwa ajili ya vijana. Inawezekana tu kuwa na ujana ikiwa wewe kama mwanahabari kijana unaongoza mchakato kupitia kila hatua ya matayarisho. Hatua muhimu ni show clock, inayoonyesha jinsi kipindi chako kimetengenezwa. Chini kuna ratiba ya kipindi cha COVID-19 cha dakika 60. Ikiwa kipindi chako kina urefu wa dakika 30, punguza idadi ya miundo itakayochezwa kwenye makala:

UTANGULIZI WA KIPINDI: MADA NA MUHTASARI WA KIPINDI

Muundo 1: SAUTI ZA UMMA

Kufungua kipengele cha 'diary ya sauti'

Muundo 2: 'DIARY YA SAUTI'

Kufunga kipengele cha 'diary ya sauti' na ufungue kipengele cha mahojiano

Muundo 3: MAHOJIANO

Funga kipengele cha mahojiano

Muundo 4: JE, WAJUA?

Fungua kipengele cha maoni ya sauti

Muundo 5: MAONI YA SAUTI

Funga maoni ya sauti na ufungue kipengele cha wasifu wa sauti

Muundo wa 6: WASIFU WA SAUTI

Funga kipengele cha wasifu wa sauti

Muundo wa 7: JE, WAJUA?

Onyesha wasikilizaji: Waelekeze wasikilizaji kuungana nawe kwenye mkondo wako wa moja kwa moja kwenye Facebook kwa maswali na majibu na kushiriki kwenye jaribio (lililorekodiwa)

- Miundo ya sauti



kwa sehemu ya maelezo zaidi kwa kila moja.

- Kufungua na kufunga miundo



kwa sehemu ya miundo kwa maelezo ya jinsi ya kufungua na kufunga miundo

WhatsApp ndio jukwaa la msingi la kurekodi na kushirikisha. WhatsApp ndio inapaswa kutumiwa kama jukwaa la kutuma vipengele vya kipindi cha redio kwa mwezeshaji na timu ya CRF/MYCN. 'Show clock' inaweza kutumwa kupitia WhatsApp kama pdf, hati ya maneno, picha au kama ujumbe wa maandishi. Kilicho muhimu zaidi ni kuhakikisha kwamba umeweka utambulisho unaofaa na kuandaa vipengele vyako vya redio vizuri kwa pamoja unapotumia mwezeshaji na timu ya CRF/MYCN.

Wakati wa kutoa vipengele vya kipindi cha redio' na mwezeshaji na timu ya CRF, jambo muhimu ni kuhakikisha kuwa maandalizi yako yote yameandikwa kwa

usahihi. Faili zote zinapaswa kusema wazi mada, jina la kipindi, tarehe ya kipindi na yaliyomo, kama ifuatavyo:
COVID-19_JINA LA KIPINDI_TAREHE _
YALIOMO KWENYE KIPINDI



ikiwa wasifu wa sauti unaunda sehemu ya 'kipindi chako cha redio', ungependa kuweka kumbukumbu ya wasifu kama ifuatavyo:
COVID-19_PREVENTION_16 APRIL 2020_WASIFU WA SAUTI. Ikiwa unaweka 'show clock', itakuwa na alama kama ifuatavyo: COVID-19_KINGA_16 APRIL 2020_SHOW CLOCK

KUHIFADHI KIPINDI KWENYE MTANDAO WA SOUNDCLOUD

COVID-19 ni janga la kote ulimwengu na ni muhimu kwamba unayoandaa yataweza kupokelewa na kusikilizwa na hadhira iliyopo zaidi ya jamii yako tu. Kwa njia hii unachangia mazungumzo ya ulimwenguni kote na mapendekezo ya suluhisho kusambazwa katika majukwaa na mashirika tofautii.

Ili CRF/MYCN iweze kupata vipindi vya redio, vinahitaji kuhifadhiwa kwenye mtandao wa SoundCloud (www.soundcloud.com).

SoundCloud ni jukwaa rahisi la kuweka vipindi vya redio au miundo ya redio, na kuvifanya kuwafikia hadhira kubwa. Kwa kuwa ni ngumu kutuma faili kubwa la sauti kupitia barua pepe, basi unaweza kutumia SoundCloud. SoundCloud hukuruhusu kupakia miundo yako ya redio na kuwasilisha maelezo kwa kila moja. Vipindi au miundo yako ya redio itapakiwa kwenye ukurasa wa kikundi cha "YRN (Tanzania)" kwenye mtandao wa SoundCloud, ambapo sisi, waandishi wengine, vituo vya redio, au umma tunaweza kusikiliza vipindi vyako na miundo tofauti, kupakua, kuzirusha

kupitia Facebook au Twitter, au hata kutoa maoni kuhusu kile ambacho umeandaa.

Kama ilivyotajwa katika sehemu ya 'Ugawaji wa majukumu ya kikundi', kuhifadhi vipindi ni jukumu la mwezeshaji na kazi watakayotimiza watakapokuwa wamemaliza kuandaa kipindi. Lakini ni jukumu la watayarishaji wa kipindi waangalie tena kuhakikisha kwamba kipindi ambacho kilitengenezwa kilipakiwa na kuhifadhiwa kwenye mtandao wa SoundCloud.

Iwapo mtayarishi wa kipindi anaweza kupata kompyuta na njia za kupokea kipindi kilichlorekebishwa kupitia huduma za mtandao za uhamishaji, basi anaweza kuchukua jukumu la kupakia nakuhifadhi kipindi hicho kwa mtandao wa SoundCloud.

Hapa kuna hatua za kufuata unapohifadhi vipindi kwenye SoundCloud:

- Hakikisha kuwa programu yako ni faili ya mp3. Hii hufanya faili kuwa dogo na rahisi kuituma mtandaoni. Ikiwa sio faili ya mp3,

tumia iTunes au kicheza sauti kingine ili kuibadilisha iwe mp3.

- Nenda kwenye <https://www.soundcloud.com/>, ujisalili na uingie
- Nenda kwenye tovuti hii: <http://soundcloud.com/groups/youth-radio-network-south-africa>
- Bonyeza kitufe cha “Pakia”.
- Bonyeza kitufe cha “Chagua faili”.
- Chagua faili la sauti unayotaka kupakia na bonyeza “Fungua”. Hapa ndipo umuhimu wa kuweka kumbukumbu unapokuja. Kwa wakati huu, itaanza kupakia kiotomatiki. Unaweza kufuatilia maendeleo kwenye skrini yako kwa mstari wa bluu unavyo songa mbele. Wakati mwingine, ikiwa unganisho lako la mtandao litakatika, basi haitafaulu. Jaribu tena tu.
- Baada ya kumaliza kupakia, itapitisha faili, ambapo inamaanisha kwamba imebadilishwa ili iweze kutumika kwenye SoundCloud.
- Andika jina la kipindi. Tumia muundo huu:

Jina la Kikundi cha Redio (“Sauti ya Vijana”): Mada (“COVID-19”). Anza kila wakati na jina la kikundi chako, ikifuatiwa na mada ya kipindi cha redio / kipengele unachopakia.

- Bonyeza kwenye “Picha” ili kupakia picha inayohusiana na kipindi au fomati - hii ni lazima. Lakini, ukiamua kupakia picha, hakikisha inafaa katika kipindi cha redio au miundo na haivitoi vibaya au kuweka wageni waliomo hatarini.
- Ambapo inasema ‘vitambulisho’, weka maneno ambayo yanahusu muundo au kipindi chako.
- Chini ya “Maelezo” andika aya fupi inayoeleza muundo au kipindi kilichomo. Wape wasikilizaji wako habari ambayo unafikiri wanahitaji kuwa nayo na uzingatie kwamba watangazaji wengine wanaweza kupendezwa na kurusha kipindi chako pia, kwa hivyo wanaweza kuhitaji habari zaidi kuliko vile unavyofikiria.

5. SHUKRANI

CRF/MYCN ingependa kukushukuru kwa upokeaji wako kwa mbinu ya kuripoti tokea nyumbani na zana ya utangazaji ili kukabiliana na janga la COVID-19.

Tunatazamia kuona njia za ubunifu ambazo utaweza kutumia kupambana na vizuizi ambavyo unakutana navyo na kupokea mafunzo haya ili kuyatoa katika mtandao wowote. Tunatarajia haswa kusikia hadithi za jamii ambazo utaweza kupata na kutoa za COVID-19.

Kaa salama. Kaa ukiripoti.

RASILIMALI

Rasilimali za COVID-19:

- Ya Kimataifa kutokwa kwa Shirika la Afya la Duniani
Global WHO COVID 19
- Kile wahuduma wa afya wanachopaswa kujua kuhusu kushughulikia wagonjwa au wanaoshukiwa kuwa na maambukizi ya COVID-19
What Healthcare Personnel Should Know about Caring for Patients with Confirmed or Possible COVID-19 Infection | CDC
- Kujitenga au kutengwa
Self isolate or quarantine_Al Jazeera
- <https://www.niaid.nih.gov>
- **South African Government COVID 19 site**
- **Johns Hopkins Coronavirus COVID-19 Global Cases**
- **National Institute for Communicable diseases (NICD)**
- **National Department of Health Covid 19**
- **WHO Q&A on COVID-19. Maswali na majibu ya Shirika la Afya Duniani kuhusu COVID-19**
- Muongzo wa UNICEF na WHO wa waalimu wa kulinda watoto na kuendeleza shughuli kwa usalama shuleni
UNICEF and WHO guidance for teachers to protect children and support safe school operations
- Muongzo wa virusi vya Corona
Coronavirus handbook
- Jinsi ya kuripoti COVID -19 bila kueneza hadithi potofu
How to cover COVID-19 without spreading misinformation
- **Youtube COVID-19 awareness videos. Video za Youtube za maelezo ya Covid-19**

RASILIMALI

- <https://economictimes.indiatimes.com> understanding lockdown
- <https://www.thefactsite.com/mobile-phone-facts>
- <https://www.facebook.com/groups/CapeTownTogether/about/>

Rasilimali za urushaji wa mara moja kupitia mitandao ya kijamii:

- Vidokezo 26 vya ushirikishaji bora kwenye mtandao wa Facebook
<https://www.socialmediaexaminer.com/26-tips-for-better-facebook-page-engagement/>.
- Muongozo wa matumizi ya mitandao ya kijamii
<https://radio.co/radio-university/social-media-strategy-for-radio>
- Muongozo wa mitandao ya kijamii
<https://moz.com/beginners-guide-to-social-media>